**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI TINGATINGA**

**WILAYA YA LONGIDO**

**S. L. P. 230 SANYA JUU**

**SIMU NO: +225 – 756 981466 AU +225 – 786 686019**

**Kumb Na TSS/ AD/01/VOL 10**

**Ndugu Mzazi wa**.................................................................................................

**Tarehe** ........................................................................................................

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA**

**MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Tinga Tinga mwaka huu wa 2021 kwa niaba ya walimu na Watumishi wengine wa Shule ya Sekondari ya Tinga Tinga, Nachukua fursa hii kukupongeza mwanao kupata nafasi hii muhimu. **HONGERA SANA!**

## MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Tinga Tinga iko katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Longido, Tarafa ya Enduimet, kata ya Tinga Tinga, kijiji cha Tinga Tinga.

## JINSI YA KUFIKA SHULENI

Kwa Wanafunzi wanao toka Longido, Ketumbeine,Engarenaibor, Gilai na Namanga ni muhimu wakapanda Magari toka **LONGIDO** na kuja moja kwa Tinga Tinga na Kwa wale wanaotoka Kamwanga, Lerang'wa, Olmolog nao wakaenda hadi **Sanya Juu** kabla ya Saa 5 Asubuhi Magari yatakuwepo Muhimu Mwanafunzi na Mzazi wawe na Nauli zao. **Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe . 11.01. 2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe . 25. 01. 2021 ndani ya siku Kumi na Nne (14).**

## SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

Suruali mbili (2) rangi ya Dark Blue, Suruali1 shamba dress rangi ya Nyekundu , mashati 2 Meupe mikono mifupi, tai 1 rangi ya Dark Blue yenye mistari meupe, Sweta rangi ya Dark Blue origional yenye shingo ya V, T – shirt 2 Rangi ya Nyekundu yenye kola mpya isiyo na maandishi au picha , viatu vya rangi nyeusi jozi mbili 2 na viwe vya kufunga kwa kamba, na soksi nyeusi pair mbili (2).



Scanned by CamScanner

## SARE ZA SHULE KWA WASICHANA.

Sketi 2 Rinda Boksi rangi ya Dark Blue , sketi Ishamba dress rinda boksi Rangi Nyekundu, mashati 2 meupe mikono mifupi, Tai 1 Dark Blue yenye mistari meupe, Sweta rangi ya Dark Blue original yenye shingo ya V, T – shirt 2 Rangi Rangi Nyekundu yenye kola isiyo na maandishi au picha , soksi, 2 ndefu nyeupe (stockings) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba na visiwe na visigino virefu

NB; Mzazi atakayeshindwa kuelewa rangi ya sare awasiliane na mkuu wa Shule kuepuka usumbufu wa kurudia kushona nguo.

## MAMBO MENGINE MUHIMU KWA WOTE.

1. Nguo za michezo, Bukta 1 na raba pair 1
2. Godoro 2 ½ x 3 ft x 6 ft, shuka mbili za rangi ya pinki kwa wasichana na blue bahari kwa Wavulana, Blanketi 1 na Mto 1 na Neti moja.
3. Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe na kijiko vyote vya Alluminium.
4. Ndoo 2 za maji lita 10 kwa matumizi binafsi.
5. Vifaa vya darasani madaftari yasiyopungua 15 (counter book kuanzia Quire Three), mathematical set, kalamu ya blue, black na four figure.
6. Kamusi ya kiingereza (oxford dictionary)
7. Fedha za matumizi (pocket money) kwa ajili ya mwanao na nauli kwa ajili ya wakati wa likizo kwa mwanao.
8. Track suti Rangi Nyekundu yenye mistari meupe Mikononi na Pembeni (Adidas) kwa wavulana na wasichana.

Nasisitiza kuwa ni lazima kila mwanafunzi afike na mzazi au mlezi wake siku ya kwanza ya kuripoti kwake shuleni.

- Pamoja na barua /fomu hii naambatanisha na fomu ya daktari kwa ajili ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi. Fika na Fomu hii siku ya Kuripoti
- Ni Lazima Mzazi anapomripotisha mwanafunzi awe na Nakala ya Cheti cha kuzaliwa ni Muhimu sana na Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA ya Mzazi.

Karibu Sana Shule ya Sekondari Tinga Tinga

**PANTALEO PARESSO**

………………………….

**MKUU WA SHULE**



Scanned by CamScanner

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**WIZARA YA ELIMU,SAYANSI,TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

**SHULE YA SEKONDARI TINGA TINGA**

**WILAYA YA LONGIDO**

**S. L. P. 230 SANYA JUU**

**SIMU NO: +225 – 756 981466 AU +225 – 786 686019**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE NA MASHARTI YAKE

### A. MWANAFUNZI:

Mimi ............................................................................................. Ninakubali/sikubali kujiunga na Shule ya Sekondari Tinga Tinga na kuwa tayari kufuata masharti na Sheria zote za shule.

Sahihi ..........................................................................................

Tarehe ........................................................................................

### B. MZAZI/ MLEZI:

1. Jina kamili............................................................................................
2. Kazi yake ....................................................................
3. Anwani ya Nyumbani.....................................................................................
4. Kijiji.........................................kata......................................tarafa...............
   wilaya..........................mkoa.........................uraia..................................
   ....
5. Namba ya simu ....................................................
6. Dini/ Dhehebu unalotaka mwanao afelewe.........................................................
7. Nimesoma barua ya kuripoti shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatanishwam nimeelewa na nimeridhika na ninakubali wajibu huo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kukiuka.
8. Ninaahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na walimu katika kumlea kijana wangu ili awe na tabia njema siku zote, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa mwanangu akienda kinyume na sheria za shule hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.
   Nadhibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni za kweli.

**JINA LA MZAZI / MLEZI**

**...........................................................................................................**

**SAINI................................................ TAREHE ..................................**



Scanned by CamScanner

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotelewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na ya nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (prepation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.



Scanned by CamScanner

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer

Pupil's Full name ........................................Age ..........................................

Blood count (Red or White) ..............................................................................

Stool Examination ...........................................................................................

Urine ....................................................................................................................

Syphilis test ........................................................................................................

T. B.........................................................................................................................

Eye test .................................................................................................................

Chest test...............................................................................................................

Abdomen test .......................................................................................................

Spleen test ............................................................................................................

Additional information e.g. Physical defects, infection, chronic or family diseases etc,

...................................................................................................................................
...................................................................................................................................
...................................................................................................................................
...................................................................................................................................
...................................................................................................................................
...............................................

I certify that the above is fit to pursue for further studies.

**Signature**:

...................................................................................................................................

**Designation**:.......................................................................................................

**Station**: ............................................................................................................

**Date**: ..................................................................................................................

NB: Tafadhali uje na Fomu hii siku ya kuripoti shuleni. Futa isiyohusika.



Scanned by CamScanner